Yehova, Mungu Wetu (Jehovah, Our God)

Na

Ellis P. Forsman

Yehova, Mungu Wetu

Na

Ellis P. Forsman

Octoba 12, 2011

Yehova, Mungu Wetu

Zaburi 147:3-5

Zaburi 147:3-5, "*Huwaponya waliopondeka moyo, na kuziganga jeraha zao. Huihesabu idadi ya nyota, huzipa zote majina. Bwana wetu ni mkuu na mwingi wa nguvu, akili zake hazina mpaka.*"

Katika maisha ya wanadamu, tunapenda kuona matukio ya uelewa, huruma, ukarimu, upendo, na uungwana. Tunapofanya mambo haya tunafikiria hakika kwamba ni makuu au yenye nguvu.

Tunatamani ubora huu uwe katika mtu ambaye hajakamilika. Tunapaswa kumuelekezea Mungu ambaye ndiye mkamilifu na hana ukomo.

Katika kifungu chetu cha maandiko tunaona nguvu na uelewa, upole na upendo wa Mungu.

Uelewa Na Nguvu

Zaburi 147:4-5, "*Huihesabu idadi ya nyota, huzipa zote majina. Bwana wetu ni mkuu na mwingi wa nguvu, akili zake hazina mpaka.*

Nyota.

Nyota huvutia wengi wetu.

Mungu kwa Elihu katika Ayubu 38:4-7, "*Ulikuwa wapi nilipoweka misingi ya nchi? Haya! Sema kama ukiwa na ufahamu. Ni nani alieamrisha vipimo vyake, kama ukijua? Au ni nani alienyosha kamba juu yake? Misingi yake ilikazwa juu ya kitu gani? Au ni nani aliyeliweka jiwe lake la pembeni, hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa nguvu?*"

Mungu anazitambua nyota kama ni bora na muhimu.

Anafahamu idadi yao. Anafahamu majina yao.

Taarifa ifuatayo kuhusu nyota ilichukuliwa kutoka, "Nyota" na Bw James Dean, katika "*Ulimwengu kuhusu sisi*":

Nyota iliyoko karibu ina mwanga 4.27 miaka mingi huko. Mwanga husafiri kwa maili 186,000 kwa sekunde. Huchukua sura ya mwanga 4.27 kwa mwaka kusafiri kutoka katika nyota hiyo hadi duniani.

Nyota iliyoko mbali ni Njia ya Maziwa na inamwanga 220,000 miaka kutoka katika nyota hiyo.

Wanasayansi wanatuambia kuwa kuna takriban nyota milioni 1,500 katika Njia ya Maziwa – takriban nyota 200 kwa kila mtu duniani. Biblia inatuambia kwamba Mungu anajua hakika idadi ya nyota na majina ya kila mmoja.

Nyota iliyoko mbali zaidi inamwanga 140 milioni miaka kutoka kwake. Zidisha hiyo mara 5,865,696,000,000 (5 trilioni, 865 bilioni, 696 milioni) maili inachukua mwanga kusafiri kwa mwaka na una maili ngapi ya nyota iliyoko mbali zaidi kutoka duniani.

Dunia ni chini ya 8,000 maili kwa diamita.

Jua lipo maili 860,400 kwa diamita; zaidi ya mara 100 upana kama dunia.

Nyota moja, Betelguse, ni mara milioni 27 upana sawa na jua.

Mfumo wa kimaikroskopi.

Katika muelekeo mwingine, Mungu hujali vitu ambavyo ni vidogo mno. Kuna vitu visivyo hesabika ambavyo tu huweza kuonekana kwa maikroskopi, na vitu ambavyo ni vidogo sana haviwezi kuonekana kwa maikroskopi ya kawaida, kama vile atomi.

Mfumo Wa Ulimwengu Una Mlolongo – Iliumbwa

Kwa imani tunahiari kusema, "*Mungu aliitengeneza yote, na anaishikilia na kuiongoza yote.*"

- Zaburi 147:5, "*Bwana wetu ni mkuu na mwingi wa nguvu, akili zake hazina mpaka.*"
- Heb 11:3, "*Kwa imani twafahamu kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.*"

Hapa imani uungana kwa sababu.hakuna maelezo mengine ya maantiki. Kwa uchunguzi wote kuhusiana na uumbaji wa ulimwengu, kuna ufunguo mmoja tu wa maana, "*hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia.*" (Mwanzo 1:1).

Ukarimu, Upendo, Na Ukarimu Wa Mungu

Zaburi 19:1-11, "*Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, na anga laitangaza kazi ya mikono yake. Mchana husemeza na mchana, usiku hutolea usiku maarifa. Hakuna lugha wala maneno, sauti yao*

haisikilikani. Sauti yao imeenenea duniani mwote, na maneno ya hata miisho ya ulimwengu. Katika hilo ameliwekea jua hema, kama bwana harusi akitoka chumbani mwake, lafurahi kama mtu aliye hodari kwenda mbio katika njia yake. Kutoka kwake lautoka mwisho wa mbingu, na kuzunguka kwake hata miisho yake, Wala kwa hari yake hakuna kitu kilichositirika. Sheria ya BWANA ni kamilifu huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa BWANA ni amini humtia mjinga hekima. Maagizo ya BWANA ni ya adili, huufurahisha moyo. Amri ya BWANA ni safi, huyatia macho nuru. Kicho cha BWANA ni kitakatifu, kinadumu milele. Hukumu za BWANA ni kweli, zina haki kabisa. Ni za kutamanika kuliko dhahabu, kuliko wingi wa dhahabu safi. Nazo ni tamu kuliko asali, kuliko sega la asali. Tena mtumishi wako huonywa kwazo, katika kuzishika kuna thawabu nyingi."

Mungu ambaye ametangaza nguvu yake kwetu katika ulimwengu pia ametangaza upendo wake kwetu kwa kutuhudumia mahitaji yetu katika neno lake lililotangazwa. Anauwezo wa kuponya mioyo yetu iliyovunjika na kufunga vidonda vyetu.

Hatujapotea kwa Mungu. Miongoni mwa wote wanaoishi, na wamewahi kuishi, anatujua kwa majina, na anafahamu mahitaji yetu.

Mat. 6:8, "*Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba.*"

Tunapozingatia uharibifu wa ulimwengu, udogo wa dunia yetu, udhaifu wetu na ubaya wa kuanguka, tunahisi kwamba "Mungu hapendezwi name."

Daudi alijisikia hivyo. Zaburi 8:3-4, "*Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako, mwezi na nyota ulizoziratibisha; mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu hata umuangalie?*"

Alafu akakumbuka na kusema, "*Umemfanya mdogo punde kuliko Mungu; umemvika taji ya utukufu na heshima; umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umevitia vitu vyote chini ya miguu yake.*" (Zab. 8:5-6).

Tabia Ya Mwanadamu

Wewe ni mdogo; dunia yako ni sawa na kimchanga; uzima wako duniani ni sawa na mchoro wa sekunde unaolinganishwa na nyota isiyoonekana ambayo huwaka mara moja na kuzima, lakini wewe ni mkuu kuliko nyota. Mungu alikuumba hivyo.

Nyota hazijui kama zinaishi, kwamba huwaka mara moja na kuzima; lakini wewe unajua kwamba unaishi. Mungu alikuumba kwa mfano wake mwenyewe "kufahamu."

Mioyo iliyovunjika haina hekima na kuonekana kama nyota, lakini ni nyingi na zipo dunia nzima. Hutokea kwa njia ya ukorofi, isiyohaki, kuvunjika moyo, chuki, muonekano usio haki, ujanja, kushindwa na kubuni mifumo mingine.

Wasio na imani hushindwa, huwa wakali, wasio na tumaini, na wapungufu.

Wenye imani huamini, hutubu, na hutarajia.

Husema, kama Ayubu alivyokuwa, "*Tazama utaniua; sina tumaini; ila hataivyo nitaithibitisha njia yangu mbele yake.*" (Ayubu 13:15).

Mungu anapata moyo unaoamini na kutubu na kuuponya, Zaburi 34:18, "*BWANA yu karibu nao waliovunjika moyo, na waliopondeka roho huwaokoa.*"

Bwana Yesu, ambaye roho yake ilivunjika Gethsemani kwa ajili ya dhambi zetu, hupata kila moyo uliovunjika kwa sababu ya dhambi yake mwenyewe, na kuiponya.

1 Tim. 1:13-16, "*Ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri, lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani. Na neema ya Bwana wetu ilizidi sana, pamoja na imani na pendo lililo katika Kristo Yesu. Ni neno la kuwaminiwa tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi. Lakini kwa ajili hii nalipata rehema, ili katika mimi wa kwanza, Yesu Kristo audhihirishe uvumilivu wake wote, niwe kielelezo kwa wale watakaomwamini baadae, wapate uzima wa milele.*"

Hatakama mtukanaji, mtesi, na mjeruhi, mkuu wa wenye dhambi, Paulo anasema, Gal. 2:20, "*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai, wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu, na uhai nilio nao sasa katika mwili ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*"

Anakufahamu, anakupenda na akajitoa kwa ajili yako, Heb. 2:9, "*Ila twamwona yeye aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani Yesu kwa sababu ya maumivu ya mauti amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya Mungu aionje mauti kwa ajili ya kila mtu.*"

Usijali sana kuhusu matatizo na mambo ya dunia. Mungu amesema atatujali. Mat. 6:24-34, "*Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili, kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu, huwezi kumtumikia Mungu na mali. Kwa sababu hiyo nawaambieni, msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini, wala miili yenu mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?*

Waangalieni ndege wa angani ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je si bora kuliko hao? Ni yupi kati yenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja? Na mavazi ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi wala hayasokoti name nawaambia ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake hakuvikwa kama moja wapo la hayo. Basi ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba? Msisumbuke basi mkisema tule nini? au tunywe nini? Au tuvae nini? Kwa maana hayo yote mataifa huyatafuta, kwa sababu Baba yenu wa mbingini anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake, na hayo yote mtazidishiwa. Basi msisumbukie ya kesho, kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa siku maovu yake."

Hitimisho

Moyo wako unajisikiaje kwa upendo huo ambao sio wa kibinafsi na ambao ni wa kujitowa? Ebu na ikuongoze katika kumwamini na kumtii Bwana.

Rum. 2:4-6, "*Au waudharau wingi wa wema wake na ustahimili wake na uvumilivu wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu? Bali kwa kadiri ya ugumu wako, na kwa moyo wako usio na toba, wajiwekea akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu, atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.*"

Mungu amemtowa mmoja kushiriki mji wenye thamani kuliko huu. Ili kuingia katika mji huo mtu anapaswa kuwa Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si

motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* Matend 11:18, *"...Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."* Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, *"Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye."* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tuna

batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. *"Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena."* (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?